OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR

# TOLEO LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI ZANZIBAR, FEBRUARI, MWAKA 2024

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## Utangulizi

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11).


## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

## Ajali za Barabarani

Jumla ya ajali 19 zimeripotiwa mwezi wa Februari, 2024. Wilaya ya Kaskazini, "A", Kaskazini "B" na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni tatu (3) kwa kila wilaya sawa na asilimia 15.8 ikilinganishwa na wilaya nyengine


**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya, Februari 2024**




Idadi ya ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Februari, 2024 zimepungua kwa asilimia 13.6 kufikia ajali 19 kwa mwezi wa Februari 2024 kutoka ajali 22 mwezi wa Januari 2024.

Kwa mwezi wa Februari 2024, Wilaya ya Kasazini "A", Kaskazini "B" na Magharibi "B" zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi, ajali tatu (3) kwa kila wilaya na Wilaya ya Kaskazini "B", Kati na Magharibi "B" ziliripotiwa kuwa na ajali zaidi nne (4) kwa kila wilaya mwezi Januari 2024.


**Kielelezo 1.2: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani kwa Mwezi wa Januari 2024 na Februari 2024**



Idadi ya Ajali za barabarani kwa mwaka zimeongezeka kwa asilimia 46.2 na kufikia ajali 19 kwa mwezi wa Februari 2024 kutoka ajali 13 kwa mwezi wa Februari 2023.


Kwa mwezi wa Februari 2024, Wilaya ya Kaskazini “B”, Kaskazini “A” na Magharibi “B” zimeripotiwa kuwa na ajali tatu (3) kwa kila wilaya na Februari 2023, Wilaya ya Kati ilikuwa na ajali zaidi ambazo ni tatu (3).

**Kielelezo 1.3: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani Kwa Mwezi wa Februari 2023 na Februari 2024**





Jumla ya waathirika 49 wameripotiwa mwezi wa Februari, 2024, ambapo waathirika 46 walikuwa wanaume na 3 walikuwa wanawake. Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na waathirika wengi ambao ni 21 sawa na asilimia 42.9 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Februari 2024**





Waathirika waliofariki kwa mwezi Februari 2024 wameongezeka kwa asilimia 76.9 kufikia waathirika 23 waliofariki kwa mwezi wa Februari 2024 kutoka waathirika 13 waliofariki mwezi wa Januari 2024.

**Kielelezo 1.5: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Januari 2024 na Februari 2024**




Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi uliopita wamepungua kwa asilimia 3.7 na kufikia waathirika 26 waliojeruhiwa mwezi wa Februari, 2024 kutoka waathirika 27 waliojeruhiwa kwa mwezi wa Januari, 2024.

**Kielelezo 1.6: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Januari 2024 na Februari 2024**





Waathirika waliofariki kwa mwezi wa Februari 2024 wameongezeka hadi kufikia waathirika 23 waliofariki mwezi wa Februari 2024 kutoka waathirika 11 waliofariki kwa mwezi wa Februari 2023.

**Kielelezo 1.7: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Februari 2023 na Februari 2024**





Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi wa Februari 2024 wameongezeka na kufikia waathirika 26 kutoka waathirika nane (8) waliojeruhiwa mwezi wa Februari 2023.

**Kielelezo 1.8: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Februari 2023 na Februari 2024**




Mwezi wa Februari, 2024 waathirika wengi wameonekana kuwa abiria, waathirika 19. Miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani (waliojeruhiwa na waliofariki), wapanda baiskeli na pikipiki kumi na sita (16), waenda kwa miguu tisa (9) na madereva walikuwa watano (5).

**Kielelezo 1.9: Idadi na Aina ya Waathirika wa Ajali za barabarani, Februari 2024**





Kwa mwezi wa Februari 2024, ajali zaidi zilitokea muda wa saa 06:01 - 09:00 jioni ambapo zimeripotiwa ajali tano (5).

**Kielelezo 1.10: Idadi ya Ajali na Muda Uliotokea, Februari 2024**




Jumla ya ajali 19 zilizoripotiwa mwezi wa Februari, 2024, ajali 17 zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi na ajali mbili (2) zimesababishwa na uzembe wa madereva. Mkoa wa Kaskazini Unguja, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba inaongoza kwa kuwa na ajali zilizosababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi (ajali 4) kwa kila mkoa.

**Kielelezo 1.11: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa, Februari 2024**.




## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa 2,438 yameripotiwa mwezi wa Februari 2024, ambapo makosa yote yameripotiwa kwa wanaume.

Wilaya ya Magharibi "A" ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 452) sawa na asilimia 18.5 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa. Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ambayo ni makosa 51 (asilimia 2.1) kati ya makosa yote yaliyoripotiwa.


**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Wilaya, Februari 2024**




Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Februari 2024 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (**makosa 1,057**) yakifuatia Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (**makosa 497**) na Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia **(makosa 344)**.

Orodha ya makosa haya matatu (3) ya barabarani kati ya yote tisa (9) yaliyoripotiwa yamechangia asilimia 77.9


**Kielelezo 2.1: Idadi na Aina ya Makosa ya Barabarani, Februari 2024**



Idadi ya makosa kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 12.1 na kufikia makosa 2,438 kwa mwezi wa Februari 2024 kutoka makosa 2,174 mwezi wa Januari 2024.

Wilaya ya Magharibi "A" imeongoza kwa mwezi wa Februari 2024 (Makosa 452) na wilaya ya Magharibi "A" ilikuwa na idadi kubwa ya makosa kwa mwezi wa Januari 2024 (makosa 490).


**Kielelezo 2.2: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Mwezi wa Januari 2024 na Februari 2024**




Idadi ya makosa kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 3.9 na kufikia makosa 2,438 kwa mwezi wa Februari 2024 kutoka makosa 2,346 kwa mwezi wa Februari 2023.

Wilaya ya Magharibi "A" imeongoza kwa mwezi wa Februari 2024 (makosa 452) na mwezi wa Februari, 2023 wilaya ya Kusini iliongoza kwa makosa ya barabarani (makosa 409).

**Kielelezo 2.3: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa Mwezi wa Februari 2023 na Februari 2024**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11). Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 19 zimeripotiwa mwezi wa Februari, 2024. Wilaya ya Kaskazini, “A”, Kaskazini “B” na Magharibi “B” zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni tatu (3) kwa kila wilaya sawa na asilimia 15.8 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

Idadi ya ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Februari, 2024 zimepungua kwa asilimia 13.6 kufikia ajali 19 kwa mwezi wa Februari 2024 kutoka ajali 22 mwezi wa Januari 2024.

Jumla ya makosa **2,438** yameripotiwa mwezi wa Februari 2024, ambapo makosa yote yameripotiwa kwa wanaume.

Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Februari 2024 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (**makosa 1,057**) sawa na asilimia 43.4 ya makosa yote yaliyoripotiwa.

## Kiambatanisho:

**Jadweli 3.0: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Februari 2024**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nambari | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 3 | 15.8 | 2 | 1 | 3 | 13.0 | 1 | 1 | 2 | 7.7 | 3 | 2 | 5 | 10.2 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 15.8 | 3 | 0 | 3 | 13.0 | 4 | 0 | 4 | 15.4 | 7 | 0 | 7 | 14.3 |
| Kati | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Kusini | 2 | 10.5 | 3 | 0 | 3 | 13.0 | 18 | 0 | 18 | 69.2 | 21 | 0 | 21 | 42.9 |
| Mjini | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Magharibi 'B' | 3 | 15.8 | 3 | 0 | 3 | 13.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 3 | 0 | 3 | 6.1 |
| Wete | 2 | 10.5 | 3 | 0 | 3 | 13.0 | 1 | 0 | 1 | 3.8 | 4 | 0 | 4 | 8.2 |
| Micheweni | 2 | 10.5 | 2 | 0 | 2 | 8.7 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 0 | 2 | 4.1 |
| Chake chake | 2 | 10.5 | 3 | 0 | 3 | 13.0 | 1 | 0 | 1 | 3.8 | 4 | 0 | 4 | 8.2 |
| Mkoani | 2 | 10.5 | 2 | 1 | 3 | 13.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 1 | 3 | 6.1 |
| **Zanzibar** | **19** | **100** | **21** | **2** | **23** | **100** | **25** | **1** | **26** | **100** | **46** | **3** | **49** | **100** |

### Jadweli 3.1: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Februari 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | | | Waendao kwa Miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 16 | 0 | 16 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **19** | **1** | **0** | **1** | **4** | **0** | 4 | **2** | **0** | **2** | **17** | **0** | **17** | **11** | **0** | **11** | **4** | **1** | **5** | **7** | **2** | **9** | **0** | **0** | **0** |

## Jadweli 3.2: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi wa Januari 2024 na Februari 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Jan-24 | Feb-24 | Jan-24 | Feb-24 | Jan-24 | Feb-24 | Jan-24 | Feb-24 | Jan-24 | Feb-24 | Jan-24 | Feb-24 | Jan-24 | Feb-24 | Jan-24 | Feb-24 | Jan-24 | Feb-24 | Jan-24 | Feb-24 | Jan-24 | Feb-24 |
| Kaskazini 'A' | 3 | 3 | 3 | 2 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 3 | 9 | 4 | 2 | 3 | 0 | 2 | 0 | 0 | 9 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 4 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 2 | 4 | 18 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 16 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 0 | 3 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 4 | 3 | 1 | 0 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Wete | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Chake chake | 1 | 2 | 2 | 1 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 2 | 3 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| **Zanzibar** | **22** | **19** | **27** | **26** | **13** | **23** | **2** | **4** | **1** | **1** | **12** | **17** | **1** | **2** | **8** | **5** | **7** | **11** | **5** | **0** | **4** | **9** |

### Jadweli 3.3: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi Februari 2023 na Februari 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Walioathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Feb 2023 | Feb 2024 | Feb 2023 | Feb 2024 | Feb 2023 | Feb 2024 | Feb 2023 | Feb 2024 | Feb 2023 | Feb 2024 | Feb 2023 | Feb 2024 | Feb 2023 | Feb 2024 | Feb 2023 | Feb 2024 | Feb 2023 | Feb 2024 | Feb 2023 | Feb 2024 | Feb 2023 | Feb 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 3 | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 3 | 1 | 4 | 1 | 3 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 2 | 0 | 18 | 2 | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 16 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'B' | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Wete | 1 | 2 | 2 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Micheweni | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 2 | 3 | 0 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **13** | **19** | **8** | **26** | **11** | **23** | **0** | **4** | **0** | **1** | **5** | **17** | **4** | **2** | **3** | **5** | **5** | **11** | **0** | **0** | **2** | **4** |

### Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Februari 2024

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji Hatari | | | Ubovu wa Vipando | | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 19 | 0 | 19 | 0 | 0 | 0 | 35 | 0 | 35 | 62 | 0 | 62 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 6 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 | 11 | 65 | 0 | 65 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 78 | 0 | 78 | 17 | 0 | 17 | 64 | 0 | 64 | 81 | 0 | 81 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 7 | 0 | 7 | 8 | 0 | 8 | 12 | 0 | 12 | 42 | 0 | 42 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 6 | 27 | 0 | 27 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 104 | 0 | 104 | 92 | 0 | 92 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 36 | 0 | 36 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 12 | 0 | 12 | 30 | 0 | 30 | 11 | 0 | 11 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 4 | 0 | 4 | 25 | 0 | 25 | 16 | 0 | 16 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 23 | 0 | 23 | 17 | 0 | 17 | 25 | 0 | 25 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 25 | 0 | 25 | 30 | 0 | 30 | 40 | 0 | 40 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **0** | **16** | **0** | **16** | **111** | **0** | **111** | **94** | **0** | **94** | **344** | **-** | **344** | **497** | **0** | **497** |

**Inaendelea… Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Februari 2024**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 24 | 0 | 24 | 150 | 0 | 150 | 0 | 0 | 0 | 292 | 0 | 292 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 23 | 0 | 23 | 137 | 0 | 137 | 0 | 0 | 0 | 245 | 0 | 245 |
| Kati | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 29 | 0 | 29 | 34 | 0 | 34 | 0 | 0 | 0 | 307 | 0 | 307 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 99 | 0 | 99 | 3 | 0 | 3 | 178 | 0 | 178 |
| Mjini | 94 | 0 | 94 | 0 | 0 | 0 | 21 | 0 | 21 | 212 | 0 | 212 | 0 | 0 | 0 | 360 | 0 | 360 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 49 | 0 | 49 | 202 | 0 | 202 | 0 | 0 | 0 | 452 | 0 | 452 |
| Magharibi 'B' | 44 | 0 | 44 | 0 | 0 | 0 | 12 | 0 | 12 | 163 | 0 | 163 | 0 | 0 | 0 | 265 | 0 | 265 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 | 8 | 18 | 0 | 18 | 0 | 0 | 0 | 84 | 0 | 84 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 51 | 0 | 51 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 26 | 0 | 26 | 0 | 0 | 0 | 93 | 0 | 93 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 | 0 | 16 | 0 | 0 | 0 | 111 | 0 | 111 |
| **Zanzibar** | **140** | **0** | **140** | **0** | **0** | **0** | **176** | **0** | **176** | **1,057** | **0** | **1,057** | **3** | **0** | **3** | **2,438** | **-** | **2,438** |

**Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Februari, 2023 na Februari, 2024**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Februari 2023 | Februari 2024 | Februari 2023 | Februari 2024 | Februari 2023 | Februari 2024 | Februari 2023 | Februari 2024 | Februari 2023 | Februari 2024 | Februari 2023 | Februari 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 3 | 2 | 4 | 19 | 4 | 0 | 65 | 35 | 47 | 62 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 2 | 3 | 8 | 6 | 20 | 0 | 54 | 11 | 83 | 65 |
| Kati | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 78 | 25 | 17 | 26 | 64 | 71 | 81 |
| Kusini | 0 | 0 | 7 | 2 | 127 | 7 | 38 | 8 | 43 | 12 | 161 | 42 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 125 | 0 | 109 | 6 | 1 | 27 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 82 | 5 | 77 | 104 | 0 | 92 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 112 | 0 | 93 | 10 | 37 | 36 |
| Wete | 0 | 0 | 19 | 5 | 8 | 0 | 10 | 12 | 83 | 30 | 12 | 11 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 4 | 31 | 25 | 5 | 16 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 23 | 23 | 14 | 17 | 10 | 25 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 22 | 25 | 11 | 30 | 21 | 40 |
| **Zanzibar** | **0** | **-** | **32** | **16** | **147** | **111** | **462** | **94** | **606** | **344** | **448** | **497** |

**Inaendelea… Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Februari, 2023 na Februari, 2024**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Februari 2023 | Februari 2024 | Februari 2023 | Februari 2024 | Februari 2023 | Februari 2024 | Februari 2023 | Februari 2024 | Februari 2023 | Februari 2024 | Februari 2023 | Februari 2024 |
| Kaskazini 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 27 | 24 | 81 | 150 | 0 | 0 | 232 | 292 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 23 | 107 | 137 | 2 | 0 | 288 | 245 |
| Kati | 0 | 2 | 0 | 0 | 22 | 29 | 11 | 34 | 0 | 0 | 156 | 307 |
| Kusini | 0 | 0 | 22 | 0 | 0 | 5 | 11 | 99 | 0 | 3 | 409 | 178 |
| Mjini | 1 | 94 | 94 | 0 | 0 | 21 | 19 | 212 | 0 | 0 | 349 | 360 |
| Magharibi 'A' | 3 | 0 | 0 | 0 | 91 | 49 | 15 | 202 | 0 | 0 | 268 | 452 |
| Magharibi 'B' | 2 | 44 | 0 | 0 | 56 | 12 | 12 | 163 | 0 | 0 | 312 | 265 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 8 | 21 | 18 | 0 | 0 | 154 | 84 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 39 | 51 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 8 | 26 | 0 | 0 | 65 | 93 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 | 0 | 6 | 16 | 0 | 0 | 74 | 111 |
| **Zanzibar** | **7** | **140** | **116** | **0** | **233** | **176** | **293** | **1,057** | **2** | **3** | **2,346** | **2,438** |

**Jadweli 3.6: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Januari 2023 na Februari 2024**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiriana mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Januari 2023 | Februari 2024 | Januari 2023 | Februari 2024 | Januari 2023 | Februari 2024 | Januari 2023 | Februari 2024 | Januari 2023 | Februari 2024 | Januari 2023 | Februari 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 2 | 2 | 10 | 19 | 0 | 0 | 23 | 35 | 35 | 62 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 2 | 3 | 10 | 6 | 1 | 0 | 8 | 11 | 103 | 65 |
| Kati | 0 | 0 | 7 | 2 | 76 | 78 | 12 | 17 | 29 | 64 | 75 | 81 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 7 | 6 | 8 | 10 | 12 | 24 | 42 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 64 | 6 | 34 | 27 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 5 | 37 | 104 | 94 | 92 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 10 | 27 | 36 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 12 | 20 | 30 | 11 | 11 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 4 | 12 | 25 | 13 | 16 |
| Chake chake | 0 | 0 | 1 | 2 | 23 | 0 | 24 | 23 | 0 | 17 | 0 | 25 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 | 25 | 34 | 30 | 27 | 40 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **12** | **16** | **119** | **111** | **65** | **94** | **247** | **344** | **443** | **497** |


**Inaendelea… Jadweli 3.6: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Januari 2023 na Februari 2024**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Januari 2023 | Februari 2024 | Januari 2023 | Februari 2024 | Januari 2023 | Februari 2024 | Januari 2023 | Februari 2024 | Januari 2023 | Februari 2024 | Januari 2023 | Februari 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 19 | 24 | 97 | 150 | 0 | 0 | 186 | 292 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 44 | 23 | 209 | 137 | 0 | 0 | 377 | 245 |
| Kati | 11 | 2 | 0 | 0 | 0 | 29 | 58 | 34 | 0 | 0 | 268 | 307 |
| Kusini | 3 | 0 | 0 | 0 | 41 | 5 | 65 | 99 | 15 | 3 | 164 | 178 |
| Mjini | 0 | 94 | 0 | 0 | 55 | 21 | 102 | 212 | 0 | 0 | 259 | 360 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 41 | 49 | 316 | 202 | 0 | 0 | 490 | 452 |
| Magharibi 'B' | 14 | 44 | 0 | 0 | 21 | 12 | 101 | 163 | 0 | 0 | 173 | 265 |
| Wete | 3 | 0 | 0 | 0 | 9 | 8 | 0 | 18 | 7 | 0 | 50 | 84 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 5 | 4 | 0 | 0 | 0 | 35 | 51 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 12 | 26 | 0 | 0 | 70 | 93 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 | 10 | 16 | 0 | 0 | 102 | 111 |
| **Zanzibar** | **31** | **140** | **0** | **0** | **261** | **176** | **974** | **1,057** | **22** | **3** | **2,174** | **2,438** |


**Jadweli 3.7 Tozo zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya kesi, Februari 2024**

| Wilaya | Idadi ya kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 292 | 7,017,500 |
| Kaskazini 'B' | 245 | 5,057,500 |
| Kati | 240 | 4,020,000 |
| Kusini | 245 | 5,663,000 |
| Mjini | 326 | 5,955,500 |
| Magharibi 'A' | 452 | 11,379,000 |
| Magharibi 'B' | 299 | 6,877,000 |
| Wete | 84 | 1,865,500 |
| Micheweni | 60 | 1,079,500 |
| Chake chake | 104 | 2,220,000 |
| Mkoani | 107 | 2,067,200 |
| **Zanzibar** | **2,454** | **53,201,700** |

**Kielelezo1: Ajali za Barabarani za Barabarani Zilizoripoti kwa Wilaya, Februari 2024**



**Kielelezo 2:Vifo na Majeruhi Wanaotokana na Ajali za Barabarani kwa Wilaya, Februari 2024**



## Zingatia Maelezo

Ajali ya barabarani inahusu ajali yeyote inayohusisha angalau gari moja barabarani, inayotokea barabarani kwa mzunguko wa umma na angalau mtu mmoja amekufa au amejeruhiwa. Kutokana na Sheria ya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13 ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar).

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumia gari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu. Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua, 2321,
Simu: +255242231869,
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com,
Nukushi: 024223136,
MMP, Zanzibar